# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 11 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Huu ni Mkutano wa Kumi na Moja na hiki ni Kikao cha Arobaini na Saba, kama tulivyomwomba Mwenyezi Mungu tutaanza shughuli zetu kama zilizopangwa katika ratiba ya leo. Katibu tuendelee.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu ya leo inaanza moja kwa moja na maswali, swali la kwanza linaenda Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Catherine Magige, kwa niaba ya Mheshimiwa Jafo.

Na. 376

**Utendaji wa Maafisa Utumishi**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y. MHE. SELEMANI S. JAFO)** aliuliza:-

Baadhi ya Maafisa Utumishi katika Halmashauri ya nyingi hapa nchini hufanya kazi chini ya kiwango na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi yakiwemo yale ya kutokurekebishiwa stahili zao za mishahara na vyeo kwa wakati:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inabeba lawama kwa kuwakumbatia watumishi wasio na tija?

(b) Je, ni Maafisa Utumishi wangapi mpaka sasa wamechukuliwa hatua kwa uzembe huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya Maafisa Utumishi katika Halmashauri hufanya kazi chini ya kiwango na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi, yakiwemo kutorekebishiwa stahili zao za mishahara na vyeo kwa wakati. Hivyo, mtumishi yeyote wa Umma akithibitika amekiuka Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo huchukuliwa hatua za kinidhamu na mamlaka ya nidhamu kulingana na kosa husika.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka, 2002 Mamlaka ya Nidhamu kwa Maafisa Utumishi wa Halmashauri ni Baraza la Madiwani la Halmashauri husika isipokuwa kwa Wakurugenzi na Walimu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi sasa Maafisa Utumishi 10 wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa makosa mbalimbali ikiwemo kutokurekebisha stahili za mishahara na vyeo kwa wakati.

Aidha, Serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia stahili za mishahara ya watumishi unaojulikana kama *Human Capital Management Information System (HCMIS)* ambao umesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza changamoto za ulipaji wa stahili za mishahara ya watumishi wa umma.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Halmashauri zetu tuna matatizo makubwa, Watendaji wengi wa Vijiji na Watendaji wengi wa Kata wanafanyakazi chini ya viwango na wanakuwa si waaminifu, lakini badala ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu unakuta anahamishwa kutoka Kata au Kijiji hiki anapelekwa mahali pengine, na hii inatusumbua sana hasa Wabunge wa Majimbo,

Je, Serikali inasema nini katika hili, kwa sababu sasa tusipokuwa makini wananchi watakataa huu mtindo ambao mnaufanya? Naomba majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema katika jibu la msingi kwamba watumishi wote waliopo katika Halmashauri, mamlaka yao ya Nidhamu ni Baraza la Halmashauri isipokuwa Walimu na Wakurugenzi tu. Kwa hiyo, kama wapo Watendaji wa Vijiji wanaofanya kazi chini ya viwango, na sisi Wabunge ni Madiwani katika Mabaraza yetu, naomba na ninaagiza kwamba tuwachukulie hatua zinazostahili. (*Makofi*)

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya ukosefu wa nidhamu wa matumizi katika Halmashauri zetu ni kutokujibu *queries* zilizopita, ambapo sasa hivi tuna *queries* za bilioni 78 katika Halmashauri zetu.

Je, Waziri amechukua hatua gani kwa Watendaji ambao bado wanakataa kujibu *queries* za *CAG?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, sijui kama tumeelewa *queries* ama, nadhani hizo ni hoja za Mkaguzi Mkuu wa Serikali.(*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba ukiacha Mkurugenzi, Watumishi waliobaki ni Baraza la Madiwani. Sasa tumefanya nini kuhusu wale ambao hawajajibu hoja za Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tulikuwa Morogoro tulikuwa na Wakurugenzi, lakini pia tulikuwa na kikao kingine Morogoro na Wenyeviti wa Halmashauri, katika kikao kile alikuja Mwakilishi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, na tulikuwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

Tumepitia hayo yote na Halmashauri zote tunavyozungumza sasa hivi, tayari walishajibu hoja, zimeshaletwa kwenye ofisi yangu na kabla ya Bunge hili kuisha nitakuwa nimeziweka mezani.

**MWENYEKITI:** Swali fupi sana la nyongeza la mwisho Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wka kunipa fursa nimwulize Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Kwa mujibu wa maelezo ambayo ameyatoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ni kwamba, tukitoa Mkurugenzi na Walimu, watumishi wengine waliosalia kwa maana ya Wakuu wa Idara wanapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na Mabaraza ya Madiwani, lakini rekodi zinaonesha wazi kwamba baadhi ya Mabaraza hapa nchini yameshindwa kuweza kutimiza wajibu wao ipasavyo na hivyo kupelekea matatizo mbalimbali ikiwemo ubadhirifu wa fedha.

Waziri unaweza ukalieleza Bunge letu kwamba, hakuna mamlaka nyingine mbali na Baraza la Madiwani kuweza kuwawajibisha baadhi ya watendaji ambao wameonesha *low performance* na hivyo kupelekea matatizo ndani ya jamii yetu au una *stick* kwenye utaratibu au majibu ambayo ulikuwa unasema kwamba Baraza ndilo lenye mamlaka ya kuweza kuchukua nidhamu za Watumishi na hakuna mamlaka nyingine.

Je, unaweza ukatueleza kwamba ndiyo msimamo wako?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, lakini hakuna utaratibu wa swali a na b, Waziri utajibu kwa jinsi vile unavyoona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge tujaribu kuweka maswali yetu *straight* ili yaeleweke, hatuna Kanuni inayoruhusu (a) na (b).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba, hii ni sheria ya Na. 8 ya Utumishi wa Umma inaonesha kila Mtumishi nani atamchukulia hatua. Wapo watumishi ambao mamlaka yao ya kuwachukulia hatua ni Rais, wapo ambao ni Makatibu Wakuu, wapo ambao ni Waziri wa TAMISEMI na wapo ambao wanachukuliwa na Mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo mtatuthibitishia kwamba mmeshindwa, maana yake kama Baraza lako Mheshimiwa Machali limeshindwa kufanya kazi, maana yake na wewe umeshindwa.

Pale mtakapotuletea kwamba mnakubali kwamba mmeshindwa hakuna mnachoweza kufanya hatua tutakayochukua sisi ni kuvunja Baraza.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Kasikila utaratibu ni kwamba unasimama mwanzo, usisubiri mpaka maswali yamepamba moto ndiyo unasimama katikati.

Na. 377

**Fedha za Maendeleo ya Jimbo**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO)** aliuliza:-

Je, utaratibu wa fedha za Maendeleo ya Majimbo zinazokwenda Zanzibar ukoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kujibu swali Namba 377 lililoulizwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa utangulizi kwamba mfuko wa Maendeleo ya Jimbo umeanzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Sheria Na.16 ya mwaka 2009. Sheria hiyo imemtaja Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kuwa ndiye mratibu wa mfuko huu kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo ni kuwa, kila mwaka wa fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais hupokea fedha za Maendeleo ya Majimbo kutoka Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya Majimbo yaliyopo Zanzibar.

Baada ya kupokea fedha hizo, Ofisi ya Makamu wa Rais huzipeleka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya

Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo huziwasilisha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambayo husambaza fedha hizo kwa Halmashauri za Wilaya ili zigawanywe kwa Majimbo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza sina budi kumshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa ambayo yana mtiririko uliopangwa kwa sheria zilizopitishwa na Bunge.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mfuko wa Bunge unaishia kwenye Halmashauri za Wilaya ndivyo ulivyotueleza kwa upande wa Zanzibar.

Je, Wilaya za Zanzibar zilipewa elimu ya kutosha jinsi ya kuweza kuzisambaza fedha hizi badala ya kuwahangaisha Wabunge?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mbunge mhusika anapokuwa anatimiza shughuli zake katika Jimbo kwa kutumia Mfuko wa Jimbo, wakati mwingi fedha hizo Halmashauri inakuwa inamhangaisha, inakuwa nenda rudi na wakati anapozipata karibu mwaka unamalizika, na anapoanza ule mradi zile fedha anakuwa hajazipata kikamilifu. Je, zile fedha anaweza akamaliziwa wakati mwaka wa fedha umemalizika badala ya kurejea Serikalini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika utekelezaji wa suala hili, tuligundua kwamba kuna Halmashauri ambazo zilikuwa zinafanya kinyume na sheria inavyosema.

Kwa kuanzia tulianza kutoa elimu kwa Wabunge wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi Unguja. Lakini ni lengo letu pia kuelekea katika Halmashauri za Pemba kwa sababu nako pia kuna malalamiko ya kiasi fulani. Kwa hiyo, elimu tumeanza kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fedha zinazobakia mwisho wa mwaka kama Mbunge hakumaliza kutumia, kuna kifungu cha sheria kinazungumza kwamba kama fedha itabaki, haikumalizika kutumika basi fedha ile inakuwa *carried forward* mwaka unaofuata.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili limejikita Zanzibar, kwa hiyo nafikiri niwape Wabunge wa Zanzibar kwa sababu Mbunge wa Bara sidhani kama anaweza kuwa na uzoefu wa haya yanayoulizwa Zanzibar. Kwa misingi hiyo nitampa Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ni kichocheo kinachopelekwa katika Jimbo ili kumwezesha Mheshimiwa Mbunge aweze kufanya shughuli za maendeleo katika Jimbo lake.

Lakini inavyoeleweka Zanzibar na hasa katika kisiwa cha Pemba ni kwamba mfuko huu haumhusu Mbunge.

Je, Waziri anaweza akalieleza Bunge hili, ni nani mhusika wa Mfuko huu, kati ya Mbunge na Halmashauri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, unaongozwa na sheria, lakini pia kuna Kanuni zinazoambatana na sheria hizi. Ningeomba Wabunge wazisome sheria na Kanuni hizi na wakae kitako na Halmashauri zao ili kuelezana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tulichokigundua tulipokwenda Wilaya ya Magharibi ni kwamba kuna upungufu wa uelewa wa sheria na Kanuni hizi kwa Wabunge pia kwa Halmashauri.

Kwa hiyo, Wabunge tutakapojua kanuni hizi na sheria hii, tunaweza tukafuatilia haki zetu sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo ni kwamba ofisi yangu bado inaendelea na ratiba ya kutoa elimu kwa Halmashauri. Lakini mpaka tarehe hii, kama Mbunge unauliza mfuko huu unamhusu nani basi kuna walakini kidogo.(*Makofi*)

Na. 378

**Kujenga Soko la Viwanda Mji wa Sirari**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE)** aliuliza:-

Wilaya ya Tarime inapakana na nchi ya Kenya na ina mpaka maarufu wa Sirari:-

(a) Je, Serikali itajenga lini soko la Kisasa Sirari ili kuweka mazingira ya kibiashara kati ya Tanzania na Kenya?

(b) Je, kwa nini Serikali isiufanye Mji wa Sirari kuwa ukanda wa viwanda ili kuleta ushindani na Kenya?

(c) Je, wananchi wa Tarime wananufaikaje na soko la pamoja na Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2013/2014 masoko matano (5) ya mipakani katika Wilaya za Karagwe, Ngara, Kahama na Tarime yatajengwa, likiwemo soko la kisasa la Sirari katika Kijiji cha Remagwe huko Tarime.

Tenda ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa soko la Sirari limefunguliwa jana tarehe 10 Juni, 2013 na ujenzi wa soko unatarajia kuanza mwezi Julai, 2013. Mradi huo utatekelezwa kupitia mradi wa Uwekezaji wa Kilimo(*DASIP*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ndiyo inayotarajiwa itenge eneo la kutosha karibu na Mji wa Sirari na kulikabidhi kwa Mamlaka ya *EPZ* ili liweze kuendelezwa na kuleta ushindani kama kituo cha kisasa cha viwanda na biashara kati ya Nchi yetu na Kenya.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo ya Serikali kwamba wananchi wa Tarime wananufaika na soko la pamoja na Afrika Mashariki na wanaendelea kunufaika na ruhusa ya kufanya biashara bila vikwazo vyovyote kama ilivyopitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(d) Aidha, wananchi wa Tarime wataendelea kunufaika zaidi na fursa za soko la kisasa la kimataifa katika kijiji cha Ramagwe kilichopo katika mpaka wa Sirari litakapokamilika. Wananchi wa Tarime waweke mazingira mazuri ya kupokea soko hilo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini sijui kama anafahamu kwamba iliyokuwa Wilaya iligawanywa na kuwa Wilaya mbili, Wilaya ya Karagwe pamoja na Wilaya ya Kyerwa. Sasa katika jibu lake la msingi anasema kwamba soko litajengwa katika Wilaya ya Karagwe. Sijui kama anamaanisha Karagwe au anamaanisha Kyerwa na kama ni Karagwe basi ni Kituo kipi katika Wilaya ya Karagwe?

Swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya Tarime pamoja na Wilaya ya Karagwe ni maarufu sana katika ulimaji wa zao la ndizi. Mara nyingi Serikali imekuwa ikiahidi kutafuta wawekezaji katika kuhakikisha kwamba zao hili linapata soko. Nilitaka nifahamu.

Je, Serikali imefikia wapi katika mikakati na mpango mzima kuhakikisha kwamba zao la ndizi linapata soko?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa uhakika wa soko la Karagwe ni kwamba katika Karagwe kama ni Wilaya kuna masoko mawili. Kuna soko la Mkenda na soko la Mrongo. Hayo ndiyo yanazongumziwa kwamba yatajengwa.

Kuhusu kilimo cha ndizi katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kama utapenda kilimo zaidi cha kusindika mazao kama vile ndizi au matunda na kupata labda *juice* au vinginevyo.

Nashauri kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba Halmashauri zote nchini ziweze kuwa na uwezo wa kutenga maeneo ambayo yatawakilishwa kwenye *UPZ* ili yaweze kuvutia na wawekezaji wawepo waweze kusindika mazao kama hayo ndizi, au matunda na kupata *juice* kwa ajili ya viwanda mbalimbali.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Asante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika swali la msingi imezungumzia kuanzisha viwanda katika Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu sana kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Ningependa kujua sasa nini mikakati wa Serikali kuanzisha viwanda katika mikoa mipya ikiwemo Mkoa mpya wa Geita?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Halmashauri hasa ndiyo itakayohusika kwamba Halmashauri iwe ya Wilaya yoyote au jimbo lolote lazima itenge maeneo ambayo yatakuwa ya kutoshakwa ajili ya kujenga viwanda na kwa ajili ya kufanya biashara. Kwa hiyo Halmashauri ndiyo hasa inayoanza kushughulikia suala la viwanda kwa kutenga eneo.

Serikai kupitia Wizara itatoa msimamo wa kuhamasisha wananchi na wananchi wawe tayari kuweka mazingira mazuri ya kupokea viwanda hivyo. Lakini Halmashauri ndiyo hasa hasa inayohusika kwanza.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mji wa Namanga ni mji ulioko mpakani na mlango mkubwa wa biashara kati ya Kenya na Tanzania.

Je, kwa nini Serikail haikuweka katika mipango kati ya haya masoko yanayojengwa mipakani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Namanga ni sehemu ya mpaka na ni kwamba mpakani sasa hivi Serikali ina utaratibu wa kujenga masoko mipakani.

Kwa mfano Shinyanga kule mpakani kule tunajenga soko la Busoka. Kigoma kule tunajenga soko la Mnanila. Mara kule tunajenga Sirari, soko la mpakani na Kagera huko tunajenga masoko manne hivi ya mpakani yakiwemo Mkenda, Mrongo, Kabanga, Mtukula na kadhalika.

Kwa hiyo Serikali ina utaratibu muafaka wa kujenga masoko kila mpaka.

Na. 379

**Fedha za Kuwasomesha Watanzania Fani ya Mafuta na Gesi**

**MHE. EZEKIA D. WENJE (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

Makubaliano ya uzalishaji kati ya Serikali na Kampuni ya *TPDC* pamoja na makampuni mengine ya mafuta na gesi yanaonyesha kuwa makampuni hayo yanatakiwa kulipa ada ya dola za Kimarekani 150,000 kila mwaka kwa ajili ya kusomesha Watanzania ili wawe na uelewa mpana katika sekta ya mafuta na gesi:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi hadi sasa wamekwisha someshwa kwa fedha hizo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekwisha kusanywa hadi sasa na kutoka makampuni mangapi?

(c) Je, makampuni mangapi yanastahili kuwepo katika mpango huu na fedha hizo zinasimamiwa kwa utaratibu gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mafunzo kwenye mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta *(PSA)* ipo kwenye kifungu cha 18 kinachohusu Ajira, mafunzo, ubadilishanaji wa taaluma cha mikataba ya *PSA* ambapo kila kampuni inatakiwa kulipa kiasi cha fedha kulingana na

makubaliano kwa ajili ya kusomesha wataalam wa *TPDC* na Serikali kwenye sekta ya mafuta na gesi hapa nchini. Idadi ya wafanyakazi waliosomeshwa katika ngazi mbalimbali kupitia mfuko huu wa fedha za mafunzo za *PSA* ni kama ifuatavyo; Shabaha za Uzamivu na Uzamili ni watu 27, mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ni watu 150, mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi ni watu 24 kwa gharama ya jumla ya dola za Marekani milioni 6.6.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikataba ya utafutaji wa mafuta kila kampuni inatoa kiwango tofauti cha fedha kuchangia mafunzo katika sekta ya mafuta na gesi. Kiwango hiki hutokana na makubaliano kati ya Serikali, *TPDC* na mwekezaji kwenye eneo husika la utafutaji wa mafuta na gesi.

Idadi ya makampuni yaliyopo nchini yenye mikataba ya utafutaji wa mafuta na gesi ni 25, ambayo hadi sasa yamechangia kiasi cha dola za Marekanki 12.4 milioni.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni yanayostahili kuwepo katika mpango huu ni 25 na fedha hizo zinasimamiwa kwa utaratibu wa 50/50, baina ya Serikali na *TPDC.*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Nina maswali mawili madogo. Swali la kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti, *interest* ya hili swali nilikuwa nataka kujua kwamba katika haya makampuni hayo uliyotaja 25 ni mangapi yamelipa hicho kiwango kilichopo kwenye mkataba na mangapi hayajalipa?

Kwani taarifa zilizopo ni kwamba kuna makampuni kadhaa hayajalipa, kwa sababu *figure* iliyotolewa ya dola milioni 12 ni *figure* ya jumla. Sasa tunahitaji kujua kwamba ni makampuni mangapi hayajalipa hiyo tozo kulingana na mkataba tulivyokubaliana.

Swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, hii gharama ya milioni 6.6 dola za Kimarekani kusomesha watu 27 kwa sababu wengine ni watu ambao wamepata *short courses* ni gharama kubwa sana. Inawezekana gharama ni kubwa kwa sababu gharama ya mafunzo pia ni kubwa.

Sasa kwa nini Serikali sasa isione kwamba ni muhimu kuimarisha KItengo kwa mfano cha Jiolojia cha *University of Dar es Salaam* ili waletwe wataalam kutoka nje kwa kutumia hizi fedha zilizopo ili wanafunzi wengi na wananchi wengi Watanzania wapatiwe mafunzo hapa hapa ili kupunguza gharama?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza linauliza makampuni mangapi yamelipa na mangapi hayajalipa. Kwenye majibu yangu hapa nina orodha ya makampuni yote 25 kwa *interest* ya muda nisingeweza kuyasoma yote.

Lakini niombe tu nitaikabidhi hii orodha kwako Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Mbunge ataweza kupitia hapa kampuni moja baada ya nyingine kama orodha yetu na michango ambayo wametoa inavyoelekeza.

Sehemu (b) anauliza kwamba ni gharama kubwa sana. Ni sekta ya gesi ni sekta yenye utaalam mkubwa sana na mafunzo yake si mafunzo kama mafunzo ya sekta zingine yanahusu gharama kubwa za mafunzo na yanahusisha kuwaweka watu wetu katika makampuni makubwa mengine ambayo yana uzoefu mkubwa wa kujifunza ili waweze kujifunza kwa vitendo.

Tayari Chuo Kikuu cha Dodoma kina Kitengo cha mafunzo ya mafuta na *petroleum* na wanafunzi wako pale wanasoma na wanasomeshwa na Serikali.

Kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha ili tuweze kuongeza wanafunzi wengi zaidi waweze wanaandikishwa katika kusomea mafuta na gesi katika Chuo cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha Jiolojia pia ni cha siku nyingi. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alikuwa mkufunzi pale.

Kwa hiyo tutaendelea kuongeza Bajeti yetu ya mafunzo ili Watanzania wengi waweze kujifunza hapa nchini. Lakini pia tutaendelea kuwapeleka nje ili waweze kupata ujuzi zaidi katika sekta hii ya *oil* na gesi.

Na. 380

**Huduma ya Umeme – Ludewa**

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA (K.n.y. MHE. DEO H. FILIKUNJONBE)** aliuliza:-

Serikali kupitia Waziri wa Nishati na Madini wakati akijibu swali la nyongeza kwa swali Na. 390 iliahidi kusogeza umeme kwa wananchi wa vijiji vya Ludewa Vijijini na Kijiji cha Luwana toka Ludewa Mjini:-

(a) Je, utekelezaji wa jambo hilo umefikia wapi?

(b) Je, ni lini wananchi hao watapata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge Ludewa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza miradi ya umeme katika vijiji vya Ludewa Vijijini na Kijiji cha Luwana. Miradi hii inahusisha kazi za ujenzi wa njia za umeme wa misongo mbalimbali, kufunga *transfoma* na kuunganisha wateja. Mradi wa Ludewa Vijijini ulianza kutekelezwa mwezi Desemba mwaka 2012 na wateja wa awali 232 wataunganishwa.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *KV 11* wenye urefu wa km 5, kujengwa kwa km.1.2 kati ya 2.5 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 0.4,* kufunga *transfoma* moja (1) ya *KVA 50* kuwaunganisha wateja wa awali 14. Gharama ya mradi huu ni shilingi milioni 223.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kijiji cha Luwana na vijiji vya jirani, kazi ya kupeleka umeme ilianza mwezi Aprili mwaka 2013 na katika hatua za utekelezaji wa mradi huu tayari *survey* ya km 16 na uchimbaji wa mashimo ya nguzo za umeme wa msongo wa *KV 11* yamekamilika na nguzo zimeshafikishwa katika eneo la mradi.

Mradi huu utawaunganisha wateja wa awali 700, gharama za kazi hiyo ni shilingi milioni 552.1.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa Vijijini na Kijiji cha Luwana watapata umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka huu 2013.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Naishukuru Serikali kwa jitihada za kupeleka umeme katika Wilaya ya Ludewa na hususan kijiji cha Luwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kijiji cha Luwana kimepakana na vijiji vingine vilivyopo katika Wilaya ya Nyasa, Vijiji kama Lituhi, Kiagara, Mbaha na kadhalika.

Je, Serikali ni lini itapeleka umeme katika Wilaya ya Nyasa ili vijiji hivi viweze kupata umeme?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imeshaanza mchakato wa kupeleka umeme katika Mkoa wa Ruvuma hususan Wilaya ya Songea na maeneo mbalimbali yaliyoko Mkoa wa Ruvuma na Kusini kwa ujumla.

Je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Wilaya zake ni lini umeme wa gridi hii ya Taifa kutoka Makambako kwenda Songea utawaka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwenye Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Waziri alisema hapa kwamba sasa tunaanza safari ya kwenda vijijini.

Kwa hiyo na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nafurahi kusikia kwamba sasa tunazungumzia vijiji na siyo Wilaya tena. Miradi na vijiji viko vingi si rahisi mimi kukumbuka kijiji kimoja kilichomo kwenye mpango wetu ambao tuliuwasilisha hapa.

Nimwombe Mheshimiwa Mbunge atazame orodha ile ambayo tuliitoa ya vijiji vyote vya Tanzania kama vijiji vyake vimo, kama havimo nimwahidi kwamba tutavihusisha katika mpango unaofuata kulingana na Bajeti ambavyo tunapata. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mbunge anauliza kuhusu mradi wa Mbinga-Makambako kuunganishwa kwenye gridi. Tumetenga fedha kwenye Bajeti yetu ya mwaka huu na mradi huu utatekelezwa kulingana na Bajeti tulivyokuwa tumeipangilia. Ahsante sana.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa kupeleka umeme vijijini ni maendeleo endelevu kwa Taifa letu na unapopeleka umeme nguzo zinapowekwa inakuwa ni mita 30 kwa 30 eneo la miundombinu hii ya umeme.

Je, maeneo yote yanayopita umeme vijijini Wizara imejiandaaje kutoa fidia kwa wananchi wa Babati Vijijini eneo la Dareda na Hanang Kata ya Masakita wanalalamika kwamba mashamba yao yamechukuliwa bila kupewa fidia.

Aidha wana maeneo madogo sana ya kuweza kujiendeleza kwa ajili ya kilimo chao ili iweze ikawa ni utaratibu wa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu zetu na Sheria za nchi haswa kwenye Sheria za Ardhi . Mradi wowote unakopita sehemu yoyote ama mradi wa umeme, mradi wa ujenzi wa barabara, mradi wa migodi kawaida wananchi kwenye maeneo husika huwa wanapewa fidia. *(Makofi)*

Kwa misingi hiyo *TANESCO* ndiyo inahusika na kutoa fidia za miradi hiyo ambayo kama wao *TANESCO* ndiyo wanaisimamia na kama ni miradi *REA* ambayo inasimamiwa na Wizara moja kwa moja Sheria inataka lazima fidia zilipwe. Kwa maeneo ambayo kweli mradi ule umewafuata wananchi.

Kwa hiyo mimi niombe Mheshimiwa Mbunge kama kuna wananchi wa maeneo husika hayo atupatie *I mean details* zao ili tuweze kuangalia taratibu za kisheria kama zimezingatiwa katika kutekeleza mradi huo.

Labda tu kwa taarifa tumeweza kulipa fidia katika miradi ya Shinyanga kwenye gridi ya Taifa inayokwenda Kahama kutokea pale Ibadakuli, wananchi wamelipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya nchi wananchi wameendelea kulipwa fidia na *TANESCO* kama Sheria inavyotaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tupatie orodha ya hivyo vijiji ili tuangalie kama Sheria imezingatiwa. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kujipatia nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri hapa amesema kwamba tuangalie kwenye *list* ya vijiji tulivyopewa. Naomba tu kuuliza swali la ufahamu.

Je, hilo suala halitakuwa kama mwaka jana ulitupa vijiji vingi tu. Mimi ninavyo 24 wala hata mtu kupita wa *TANESCO* hatukumwona?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi sana. Je, inakuwa ni kama mwaka jana? Ama kuna mabadiliko?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nazungumzia orodha ya vijiji ambavyo vilikuwemo kwenye Bajeti yetu ambavyo tumevitengea fedha.

Kwa hiyo sizungumzii vijiji vingine ambavyo haviko kwenye ile orodha ambayo tuliitoa ambayo viko katika Bajeti yetu. Vilivyoko kwenye Bajeti tutavitekeleza kama ambavyo tulipangilia.

Vile ambavyo vitakuwa nje ya Bajeti tutaviongeza tutaviweka katika mpango wetu kadri tunavyopata fedha na Bajeti zinazofuata kwa sababu malengo yetu sasa ni kuanza safari ya kuelekea vijijini.

Na. 381

**Misamaha ya Kodi na athari zake**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MHE. ASHA MOHAMED OMARI)** aliuliza:-

Tatizo la misamaha ya kodi limezungumzwa mara nyingi Bungeni kwamba inapunguza mapato ya nchi:-

(a) Je, ni maeneo gani yanayopata misamaha zaidi na kwa nini?

(b) Serikali imesema kuwa itaendelea na mikakati ya kupunguza misamaha ya kodi hadi asilimia 1 ya pato la Taifa.

Je, mikakati gani mahsusi inatumika na nini ni mafanikio yake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ya kodi hutolewa Kisheria kwa malengo mbalimbali yaliwemo ya kijamii, kiuchumi, kiutawala, kisiasa, kidiplomasia na kiusalama. Maeneo yanayopata misamaha kwa wingi ni vyakula muhimu, hususan wakati wa uhaba wa chakula, vifaa vya elimu, vifaa vya afya, madawa, pembejeo za kilimo pamoja na vifaa vya maji. Vyakula, elimu, matibabu na maji ni mahitaji muhimu na bila kuondolewa kodi, watu wa kipato cha chini wanaweza wakashindwa kumudu gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kimkakati kwa ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa, pia yanapata msamaha wa kodi kupitia Sheria ya Uwekezaji, inayoratibiwa na Kituo cha Uwekezaji *(TIC).* Pia, Serikali hutoa misamaha ili kutekeleza mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kijamii, kama vile Mikataba ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Mikataba ya Mashirikiano baina ya nchi mbili *(Bilateral Agreements),* Miradi ya Maendeleo, Mashirika ya Dini na Asasi za Kiraia.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati na hatua za Kiutawala, Kisheria, Kanuni na Kisera, zimekuwa zikichukuliwa ili kupunguza misamaha ya kodi isiyo ya lazima. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Baadhi ya waliokuwa hawalipi kodi ya ongezeko la thamani kupitia Jedwali la 3 la Sheria Kodi ya Ongezeko la Thamani, wanalipa asilimia kumi.

(ii) Tumefuta msamaha wa kodi ya mapato kwa makampuni yenye hisa zipatazo asilimia 25 au zaidi.

(iii) Kupunguza msamaha wa kodi ya mapato kwa makampuni yenye hisa zipatazo asilimia 25 au zaidi kutoka asilimia 20 hadi asilimia tano.

(iv) Kupunguza msamaha wa kodi uliokuwa unatolewa kwenye bidhaa zinazotambulika kama *deemed capital goods* kutoka asilimia 100 hadi asilimia 90.

(v) Kufuta msamaha wa ushukuru wa forodha kwa magari yenye ujazo wa zaidi ya *cc 3000.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hatua hizi yataonekana mara taarifa za takwimu za mwaka 2012/2013 za Pato la Taifa na misamaha ya kodi zitakapokuwa tayari. Aidha, hatua mbalimbali zitaendelea kuchukuliwa zikipunguza misamaha hiyo na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane katika hili kwa kuwa baadhi ya hatua tutakazochukua zitatugusa katika maeneo yetu.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonesha kwamba, misamaha ya kodi sasa imefikia trilioni 1.8; fedha hizi ni nyingi sana. Na katika hizo, tunapoteza bilioni 26 kwa mwaka kutokana na makampuni matano ya uchimbaji wa madini ambayo yamegoma kulipa *road toll:-*

(i) Je, Serikali ipo tayari kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kwamba, kampuni hizi zinalipa? *(Makofi)*

(ii) Iliyokuwa Kamati ya Fedha na Uchumi, iliishauri Serikali mwaka jana kufanya mapitio ya haraka ya Sheria zote na Kanuni zinazoruhusu misamaha hii ya kodi. Utekelezaji wa jambo hili umefikia wapi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misamaha ya kodi kama anavyosema Mheshimiwa Kitandula, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nimeeleza hapa Bungeni kwamba, Serikali kwa kukidhi hoja na maombi ya Waheshimiwa Wabunge mwaka jana kwamba, sasa huu ni wakati tupunguze misamaha isiyo na tija, nilieleza kwamba,

tumeanza kupitia Sheria zote. Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza maeneo ambayo ndiyo yanayopata unafuu wa kodi na sisi tunapitia Sheria, hasa zile zinazopitia kwenye *TIC* na misamaha mingine kwa mujibu wa Sheria na tutafikisha hapa ili Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kubainisha yale tuliyopendekeza, Sheria zile zibadilike zikidhi mahitaji ya kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hoja kwamba, Makampuni ya Madini yamepoteza pesa kwa maana yamekataa kulipa kodi stahiki; nachukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kodi yoyote iliyokiukwa kwa mujibu wa Sheria, Serikali tutaishughulikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda na kwa sababu Wizara hii tutaianza kesho rasmi, nafikiri bado tuna hoja nyingi za msingi, hebu tuziache mpaka kesho mniruhusu sasa tuendelee na swali linalofuata kwa kuwa tumebakiwa na muda mdogo.

Namwita Mheshimiwa Selemani Said Bungara, aulize swali lake; kwa niaba yake Mheshimiwa Rajab.

Na. 382

**Vivutio vya Kihistoria na vya Kiutalii - Kilwa**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)** aliuliza:-

Mji wa Kilwa ni wa Kihistoria, wenye vivutio vingi vya utalii kama vile magofu, minara ya wapigania ukombozi wakiwemo Omar Bin Hassan, Kinjekitile Ngwale, Makunganya na Mapango ya Nang'oma – Kipatimu:-

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa uhifadhi wa mazingira hayo na vivutio vyake vilivyoanza kubomoka?

(b) Je, fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya

ukarabati na kuboresha magofu, minara na mapango ya Nang'oma na ukarabati wa barabara iendayo maeneo hayo ili watalii waweze kufika huko kwa urahisi na kuongeza Pato la Taifa kupitia utalii wa nje na ndani?

(c) Je, Serikali, inachukua hatua zipi kutangaza vivutio hivyo vya utalii nje na ndani ya nchi kuvutia watalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilianza kuyakarabati maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kuanzia mwaka 2004, wakati ambapo *UNESCO* ilitishia kuyaondoa katika orodha ya Urithi wa Dunia na kuyaweka katika orodha ya maeneo yaliyo hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Wafadhili mbalimbali, imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuyafanyia ukarabati maeneo yote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010, jumla ya Dola za Kimarekani 100,000 kwa ufadhili wa *World Monument Fund (WMF),* zilitumika kukarabati Ngome ya Gereza la Kilwa Kisiwani. Mwaka 2011, Dola za Kimarekani 27,000 kutoka *UNESCO* zilitumika kukarabati gofu la Kasri ya Makutani – Kilwa Kisiwani; mwaka 2012, Dola za Kimarekani 266,800 kutoka Ubalozi wa Marekani, zilitumika kukarabati magofu ya Kilwa Kisiwani na Songomnara; na jumla ya shilingi 266,000,000 kutoka Mradi wa *MACEMP* zimetumika kukarabati magofu ya makaburi ya Masultani, yajulikanayo kama *Rest House* na sehemu ya Makutani ambayo haikupata fedha za ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, imewasilisha andiko la kuomba fedha katika Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* kwa ajili ya ukarabati na kuboresha magofu, minara na

mapango ya Nang'oma pamoja na ujenzi wa barabara iendayo katika maeneo hayo. Fedha hizo pia zitasaidia kutoa mafunzo ya uhifadhi na utalii, kwa vikundi mbalimbali vya jamii katika mpango uliopewa jina la *"Kilwa House of Culture."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikiandaa na kushiriki katika Maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, kama vile Saba-Saba, Nane-Nane na Wiki ya Utumishi wa Umma, ambapo wadau mbalimbali hupata taarifa na machapisho kama vipeperushi, vitabu, magazeti na *CD* zinazohusiana na vivutio hivyo. Aidha, vipindi mbalimbali vya runinga hurushwa hewani kama vile Asili ya Mtanzania kwenye *Star TV,* ZAMADAMU – *TBC 1* na Utalii wa Ndani unaorushwa katika *Channel Ten.* Pia, Wizara imekuwa ikishiriki katika Makongamano na Maonesho ya Kimataifa kwa lengo la kutangaza vivutio vya kihistoria vilivyopo hapa nchini. Mfano, ni Kongamano la Kuendeleza Utalii katika Afrika, *Tanzania Day and African Day.* Mwezi Novemba, 2012 Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wa Ufaransa Nchini, iliandaa na kuweka Onesho Maalum la Vivutio vilivyopo Kilwa katika Jengo la *Alliance Francaise,* ili kutangaza vivutio vya malikale.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(i) Pamoja na majibu ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Waziri, lakini swali la msingi ni kwamba; je, fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kukarabati na kuboresha hayo majengo? Ni kiasi gani cha fedha kimetengwa, kwa maana ninyi Serikali mmetenga kiasi gani? Hapa fedha alizozitaja zote ni kutegemea Wafadhili, hata kutengeneza makaburi! Tunataka kujua ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili hii?

(ii) Kwa kuwa Utalii unaendelea na watalii wanaendelea kuwepo; ni kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kuinufaisha Halmashauri husika ya Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbarouk, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali kama tulivyosisitiza, tumeendelea kutenga fedha ambazo nimezitaja katika matumizi ambayo yametokea tangu miaka ya 2011/2012 na 2013/2014 katika Mwaka wa Fedha uliopo. Itakuwa vigumu kumtajia kiasi kamili cha fedha, kwa sababu maeneo haya tuliyonayo nchini yanayohusiana na Vivutio vya Mambo ya Kale, yamesambaa nchi nzima na Serikali, ipo tayari kumpa takwimu ya fedha tulizoziweka katika bajeti ya mwaka huu, ili Mheshimiwa na Halmashauri husika waweze kujiridhisha kwa ushirikiano tulionao.

Mheshimiwa mwenyekiti, la pili, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, pamoja na fedha tulizopanga ambazo hazitatosha, Serikali inashirikiana na Wafadhili mbalimbali na kikubwa ni mpango wetu ambao tunafanya mazungumzo na Nchi za Jumuiya ya Ulaya *(EU)* na tunakaribia makubaliano. Makubaliano haya yatakuwa na mambo mawili; moja ni kiasi cha fedha ambazo zitatusaidia kukamilisha ukarabati wa maeneo haya ya historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya historia ni kwa ajili ya Dunia nzima. Tunasisitiza kwamba, Wananchi wote ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tujijengee utamaduni wa kutembelea vivutio vyetu vya ndani, ikiwa ni pamoja na maeneo haya ya historia tuweze kujionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tunaamini kwamba, tutakapokuwa tumeyakarabati, kitu kikubwa ni ushirikiano na kuwawezesha Wananchi wetu kuweza kufaidi vivutio hivi kwa ongezeko la biashara ya utalii wa ndani na utalii wa nje. Kama tulivyosema, vikundi mbalimbali viwe tayari, tunaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ili mapato yanayotokana na utalii yaweze ku-*trickle down* yaende kwa Mwananchi mmoja mmoja na vikundi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Khamis Kombo na mwulizaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Christowaja Mtinda. Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo waliosimama wakati swali likianza kuulizwa.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sahihisho, naitwa Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze kidogo kwa sababu sisi Watanzania tuna vivutio vingi sana vya utalii; tuna magofu, tuna bahari na tuna vilima. Ni vibaya sana kwamba, hata *Mount Kilimanjaro,* ambayo imo ndani ya Tanzania, lakini makusanyo yake ni madogo kuliko ambavyo Kenya inakusanya. Kwa nini sisi makusanyo yetu tunayokusanya Tanzania ni madogo zaidi; ni nini tatizo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna vivutio vingi ambavyo havijaweza kutumiwa ipasavyo. Ningeweza kumpa mfano; katika *Selous Game Reserve* ambayo ina ukubwa wa takribani kilometa za mraba 50000 ambayo ni sawa na nchi nyingi tu Duniani, ikiwa ni pamoja na baadhi ya nchi za Ulaya, ingeweza kutembelewa na watu wengi zaidi na watalii wengi zaidi na ndiyo jambo ambalo Serikali inafanya jitihada. Kama tulivyosema katika Hotuba ya Bajeti, iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri, kwa mara ya kwanza, mwaka jana Tanzania imeweza kufikisha watalii 1,000,000 na tunaenda tukiwakaribia sana ndugu zetu wa Kenya na watu wafahamu kwamba, pia tunashirikiana nao sana kama nchi mdau wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vivutio vyetu kama vile

Mlima Kilimanjaro, kama vile Hifadhi zetu za Taifa zote kwa ujumla wake, pamoja na haya maeneo ya mambo ya kale ambayo hayajatembelewa sana; ukizungumzia maeneo ya *Amboni Caves* na nikauliza swali hapa Bungeni ni Wabunge wangapi mlishaondoka kwa pesa zenu wenyewe bila kwenda kama Kamati, mkatembelea *Amboni Caves;* nikiomba mnyooshe mikono, mtanyoosha mikono wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba mambo mawili; moja, tunaomba tusaidiane tushirikiane kujenga utamaduni wa kutembelea maeneo yetu ya hifadhi, ikiwa ni pamoja na hifadhi zetu na vivutio vya utalii vya ndani. Pili, nimhakikishie tu Mheshimiwa Kombo, Serikali imejipanga na tunaweka jitihada za ziada tukiwa tunashirikiana na *Tanzania Tourist Board* na Wadau wengine nchini, kuhakikisha kwamba, Wananchi wanafaidi. Utalii unaleta manufaa wakati ambapo zile fedha zinaenda chini kwa watumiaji, *trickle down,* kwa hiyo, kiasi ambacho tunapata kama Serikali ni sehemu tu ya mapato ambayo yanapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Waziri, ametumia muda mrefu kujibu hilo swali. Naomba tu sasa niendelee na swali lingine.

Mheshimiwa Amina Andrew Clement, atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Amina!

Na. 383

**Utaratibu wa Kuwapeleka Vijana JKT**

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT** aliuliza:-

Kumekuwepo na wimbi kubwa la vijana walioishia Darasa la Saba na Kidato cha Nne, ambao wamekimbilia Mjini na hawana ajira za uhakika; na kumekuwepo na Mpango wa Serikali wa kuwapeleka JKT kwa mujibu wa Sheria Vijana waliomaliza Kidato cha Sita:-

(a) Je, ni kwa nini utaratibu huu wa kuwapeleka vijana JKT ulisitishwa?

(b) Je, ni sababu gani iliifanya Serikali kuamua kurudisha utaratibu huo wa JKT kwa vijana?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, utaratibu wa kupeleka vijana katika Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, ulisitishwa kwa sababu nchi yetu ilikuwa ikikabiliwa na hali ngumu ya uchumi katika kipindi cha miaka ya tisini. Wakati ule hatukuwa na uwezo wa kuwahudumia vizuri vijana hao. Kutokana na hali hiyo, Serikali ililazimika kupunguza matumizi katika baadhi ya maeneo. Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, ilikuwa miongoni mwa maeneo hayo yaliyoathirika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali imeamua kurudisha utaratibu wa kuwachukua vijana kwa mujibu wa Sheria, kwa sababu inataka kurekebisha maadili ya Vijana wa Kitanzania. Hivi sasa Serikal, imebaini kuwa maadili ya Vijana wengi wa Kitanzania yameporomoka sana. Vilevile Serikali imechukua uamuzi huu kuwajengea Vijana wa Kitanzania moyo wa kizalendo, umoja, ukakamavu na nidhamu ili hatimaye waweze kushirikiana na vijana wengine wa Kitanzania, kujenga nchi yao bila ya kujali eneo mtu analotoka, itikadi au dini anayoiamini mtu.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Amina Clement na nimewaona Wabunge walioenda Jeshini, nao pia watapata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa

Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge ni athari gani zilipatikana wakati ulipositishwa mpango huo?

(ii) Kwa kuwa Serikali imeamua kurudisha mpango huo; je, sababu zilizopelekea hapo awali kusitishwa mpango huu tayari zimeshafanyiwa ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Amina Clement, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi; moja katika athari kubwa ambazo nchi yetu imeipata kutokana na uamuzi wa kusitisha mafunzo haya ni kwamba, maadili ya Vijana wa Kitanzania yameporomoka sana. Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla, kwa nyakati tofauti tumekuwa tukilieleza jambo hili kwa uzito mkubwa sana; sasa hiyo ndiyo athari moja tumeipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, hata uwezo na dhamira ya vijana wetu wa Kitanzania katika kutumikia Taifa letu, kiwango chao kimepungua sana. Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema kwamba, tumetanabahi jambo hili ni lazima turudishe utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, zile sababu ambazo zilituzuia ili tusiweze kuimarisha mafunzo haya kwa ajili ya vijana kwa mujibu wa Sheria hivi sasa zimefanyiwa kazi? Jibu lake ndiyo. Kwanza, ndiyo maana Serikali ilibaini tatizo hilo na ndiyo maana kwa kupitia bajeti ya mwaka jana, iliamua kuanza kurudisha mafunzo hayo na utekelezaji wa jambo hilo, Waheshimiwa Wabunge, mnaujua umefikia

kiwango gani. Sasa kadiri ya hali ya nchi yetu na kwa sababu Serikali inajua umuhimu wa jambo hilo, tutafanya kila lililo katika uwezo wetu, kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha, tutenge fedha kila mwaka ili mafunzo haya yaendelee vizuri kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumejifunza kiasi cha kutosha na tutachukua hatua kwa kadiri ya uwezo wetu, kuhakikisha kwamba, tunajenga uchumi wetu ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kuhudumia vijana hawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Service Girl* Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Vijana wanaopata mafunzo ya JKT wapo kwa mujibu wa Sheria kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri, lakini pia wapo wa kujitolea ambao ni maelfu ya Vijana wa Kitanzania. Sasa kumekuwa kuna changamoto kubwa sana ya ajira, licha ya kwamba, hawa vijana wanapata mafunzo ya kijeshi. Ninafahamu kwamba, Serikali iliji-*commit* kwenye ajira za Serikali watahakikisha vijana wenye vigezo na sifa zinazostahili wanachukuliwa.

Sasa nilitaka nijue kama Serikali ina mikakati yoyote ya kuunganisha kundi hili la vijana na sekta binafsi inayohusika na masuala ya ulinzi ili hawa vijana wakimaliza masomo yale waweze kuwa *accommodated* katika ajira hizo ambazo sasa hivi zinachukua watu wengi ambao hawana hizo *skills* za kutosha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo dhamira ya kuendelea kuwapatia vijana wake ajira hasa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama na tayari imeshatoa maagizo kwa Taasisi na Wizara mbalimbali kulifanyia kazi jambo hili. Ushauri wako kwamba, Serikali lazima sasa ichukue hatua na

kuandaa mikakati maalum kwa ajili ya kuzilazimisha au kuzishauri sekta binafsi nazo zianze kuwachukua vijana ambao wamepata mafunzo ya JKT na kwa bahati nzuri vijana hawa wameandaliwa vizuri, wanayo nidhamu, wanao moyo wa uzalendo, kwa hiyo, pengine vijana hawa itakuwa ni jambo la busara sana kuwaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tutafanya kila lililowezekana kuhakikisha kwamba, Wizara zinazohusika ziwasiliane moja kwa moja na sekta binafsi ili ziweze kutekeleza jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Service Girl* Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kurudisha mafunzo na nawatakia heri Kikosi 882 - JKT Ruvu, ambao wanamaliza mafunzo yao tarehe 14 na Mungu akijalia tutaenda kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza. Tunajua wanaoenda kuna wale wanaoenda kwa mujibu wa Sheria, lakini wanaoenda kwa kujitolea kwa lengo la kupata ajira. Uzoefu unaonesha siyo wote ambao wanapata ajira katika Vyombo vyetu vya Ulinzi na moja ya mafunzo ambayo wanapata ni mafunzo ya kijeshi, ikiwepo na matumizi ya silaha.

Je, Serikali haioni kwamba wale vijana ambao wanapata mafunzo ya Kijeshi lakini wanakosa fursa ya kupata ajira, athari zake baadhi siyo wote ambao wanakuwa waaminifu na tunaona matukio yanayotokea mtaani wengine wanaenda kujihusisha na masuala ya ujambazi? Hawaoni kwamba kuna haja ya kuhakikisha wale ambao wanapata mafunzo ya matumizi ya silaha ni wale ambao watapata ajira katika Vyombo Ulinzi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya utangulizi, tunayo dhamira ya kuhakikisha kwamba, tunawaajiri vijana wote waliopitia Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kwa bahati mbaya sana, uwezo wetu wa kuwachukua vijana wote kwa wakati mmoja siyo mkubwa sana. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakati wa kuajiri vijana hawa; kwanza, tunaangalia sifa, uwezo na pia tunaangalia sifa za kiafya, maana kazi hii ya jeshi inajulikana sana kwa harakati zake na ndiyo maana inabidi lazima tuzingatie vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijana ambao tutashindwa kuwapatia ajira katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama, naziomba Wizara ambazo zinahusika na mikopo ya vijana, kuhakikisha kwamba, vijana hawa ambao tayari wamepata mafunzo ya ujasiriamali, uzalendo na nidhamu, pengine hapa ingekuwa ni mahali pazuri sana kuwapatia vijana hao mikopo, kwa sababu tayari taarifa zao zipo, maelezo yao yapo, taaluma zao zipo na uhodari wao wa kazi upo, pengine hapa itakuwa ni mahali pa zuri sana pa kuanzia. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** *Service Girl* Dokta Pudensiana.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nashukuru sana, lakini mimi siyo wale wa wiki tatu mimi nilienda mwaka mzima JKT.

**MWENYEKITI:** Haitofautishi wa mwaka mzima, wote tunaitwa *Service Girl* hata mimi pia ni *Service Girl.*

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa mafunzo haya yamerudishwa, swali langu halitatofautiana sana na la Mheshimiwa Mdee pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya. Kwamba, vijana hawa watamaliza lakini tunaona kwamba kwa mujibu wa Sheria ni wale waliofika *form six;* sasa Serikali ina mpango gani kwa hawa wanaojitolea ambao elimu yao kwa sababu moja ama nyingine haikuweza kufika hata ile ya *form four* ya cheti, ndiyo swali langu la msingi ili waweze kujikwamua na umaskini; na je, Serikali itawa-*accommodate* vipi katika shughuli za kujenga uchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeelewa swali?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pudensiana hebu nenda moja kwa moja kwenye hoja unayotaka kusema.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba; kwa kuwa wale wa mujibu wa Sheria ambao wengi wao ni *form six, diploma,* wana *skills,* lakini wapo wale wanaojitolea ambao kwa namna moja ama nyingine kwa sababu moja ama nyingine elimu yao haikuweza kufika *form four* lakini ni darasa la saba ambao pia wamejiunga. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hawa vijana wanashirikishwa katika shughuli za kujikwamua kiuchumi na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuongeza Pato la Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu; hawawezi kuunganishwa na vyuo vya ufundi hao? Basi ataendelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Kikwembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika utaratibu wetu wa kuwachukua vijana wa kujitolea katika Makambi ya Jeshi

la Kujenga Taifa, wako vijana ambao wamemaliza masomo ya darasa la saba na darasa la kumi na mbili. Sasa anauliza Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana ambao wanabahatika ambao wameonesha kwamba wanao uwezo mkubwa sana wa kufanya kazi za ulinzi, basi miongoni mwa wale vijana wa *form four* wanachaguliwa wanabahatika. Sasa kwa hao vijana ambao ni wa darasa la saba, kwa bahati mbaya sana tunao vijana wengi sana wenye sifa, kwa hiyo, pengine tunashindwa kuwachukua vijana hao. Kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya utangulizi, Serikali inao mpango, kwa sababu vijana hao tayari tunawapatia mafunzo ya ujasiriamali, tunawapatia mafunzo ya ufundi na stadi mbalimbali za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu kwamba, watakapomaliza mafunzo watapata nafasi ya kujiajiri, lakini kwa wale ambao hawakupata nafasi hiyo, pia vyuo mbalimbali vya ufundi au *VETA* kwa ujumla kama inavyojulikana, basi vijana hao wanaweza kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, kama nilivyosema, kuna suala la mikopo ambayo inatolewa na Wizara mbalimbali, pengine hapa ingekuwa ni mahali pazuri sana pa kuwapatia vijana hawa mikopo ili waweze kujiendeleza.

Na. 384

**Hitaji la Maji Kasulu Mjini**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Je, ni lini maji yatapelekwa katika Vijiji vya Heru Juu, Ruhita, Mwanga, Kidyama, Kigondo, Nyumbigwa, Karunga, Msambara, Murufiti na Nyasha ambavyo vina shida kubwa sana ya maji?

**MWENYEKITI:** Majina ya hivyo vijiji hayabadilishi maana ya swali, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya kutatua tatizo la maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Serikali ya CCM inatekeleza Mradi wa Vijiji Kumi katika Vijiji vya Nyumbigwa, Mubanga, Kasangezi, Munzeze, Nyarugusu, Rungwe Mpya, Kigogwe, Kirungu, Nyamugali na Bulimanyi. Katika utekelezaji wa Miradi hiyo, ujenzi wa miundombinu katika Vijiji vya Nyumbigwa na Mbanga ulianza na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya maji katika Vijiji vya Kasangezi, Munzeze na Nyarugusu, unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Juni, 2013. Kwa Vijiji vilivyobaki vya Rungwe Mpya, Kigongwe, Kirungu, Nyamugali na Bulimanyi, vipo katika hatua za mwisho za manunuzi na kazi za ujenzi wa miundombinu ya maji zinatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2013. Hadi kufikia mwezi Juni, 2014 utekelezaji wa Miradi ya Vijiji Kumi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014, Serikali itafufua miundombinu ya kusukuma maji kwa mashine katika Vijiji vya Karunga na Heru Juu. Aidha, baada ya kukamilisha awamu ya kwanza, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Vijiji vya Ruhita, Mwanga, Kidyama, Kigondo, Karunga, Msambara, Murufiti na Nyasha. Kwa sasa vijiji hivyo vinapata huduma ya maji kupitia miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa bomba ya mtiririko, visima virefu vyenye mtandao, visima vyenye pampu za mkono, chemchemi zilizohifadhiwa na uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Vijiji vya

Kigongo, Kidyama na Murufiti hupata maji machache kipindi cha kiangazi kutokana na Wananchi waliopo maeneo ya juu ya Miradi kujiunganishia maji bila utaratibu pamoja na kuchepusha maji kwa ajili ya mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za Serikali ya CCM kuwapatia Wananchi wa vijiji hivyo maji, namwomba Mheshimiwa Mbunge, asaidie kuhamasisha Wananchi kutohujumu miundombinu ya maji ili miradi hiyo iwe endelevu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Serikali ya CCM inafanya kazi yake, lakini na yale mabaya iwe inakubali tukiwaambia kwamba mabaya haya wanayafanya vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia suala la hujuma kwamba, niwaeleze Wananchi wanaohujumu miradi waache. Naomba niwaeleze Wananchi hao waache, lakini hujuma ambazo zinafanywa katika maeneo mbalimbali chanzo kikubwa ni tatizo la watendaji, kwa sababu watendaji wenyewe katika Halmashauri mbalimbali, wamekuwa wanahujumu Miradi hii ya Maji na *specifically* Kasulu, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo nimewahi kwenda nikakuta mabomba yaliyonunuliwa yako chini ya kiwango, wakifunga yanapasuka; hizo zote ni hujuma.

(i) Mheshimiwa Waziri upo tayari nikupeleke kwenye maeneo ambayo walifunga mabomba yakawa yanapasuka na hivyo kusababisha hasara kubwa na uweze kuwachukulia hatua baadhi ya watendaji ambao wameisababishia Serikali hasara na Wananchi kuchelewa kupata maji?

(ii) Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Mradi wa Vijiji vya Heru Juu pamoja na Karunga utaanza kutekelezwa Mwaka wa Fedha wa 2013/

2014; lakini mwaka jana ambao ni mwaka huu unaoishia Juni, zilitengwa shilingi kama milioni 85 za kuanzia. Ningependa kupata kauli ya Serikali; je, hizi fedha zitatumika au tunasubiri mpaka Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na zile fedha ambazo zilitolewa mwaka jana nazo ziko wapi? Nini kauli ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kuhusu hujuma kwamba hujuma hizi sana sana zinasababishwa na Watendaji. Mimi nadhani hili ni suala la kushirikiana, pale inapobainika kwamba ni Watendaji wanaosababisha, tukipewa taarifa tutawachukulia hatua. Ndiyo maana nimeomba hapa Mheshimiwa Mbunge utusaidie kuhamasisha kule kwako ni pamoja na kuwaambia Watendaji na Wananchi wengine wasihujumu miundombinu ya maji. Hili la kwamba utanipeleka, tupo tayari na nikitembelea nitabaini hali halisi itakavyokuwa na tunaweza tukatoa maagizo ambayo yatazingatia hali na nani amesababisha ule ubovu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Heru Juu na Kalunga, kilichofanyika ni kwamba, mwaka wa 2012/2013 tulitenga milioni 75 na siyo 85 kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge. Mradi huu gharama zake ni milioni 500. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, tunaanza utekelezaji katika mwaka huu wa 2012/2013, hizo fedha zinatakiwa zianze kufanya kazi na 2013/2014 ndiyo fedha zingine zinatakiwa zitengwe kwa ajili ya kukamilisha huo Mradi na sababu kubwa Mradi huu ni ghali kwa sababu unahusisha kupampu maji kwenye mlima siyo wa mtiririko, kwa sababu maji yanatoka chini kwenda juu; kwa hiyo, tutahitaji mashine zenye nguvu ziweze kusukuma hayo maji.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza,

nampongeza kwa kazi nzuri anayofanya ya kutatua tatizo la maji. Kama ilivyo Mji wa Kasulu, Mji wa Kigoma kuna Mradi mkubwa unaendelea; naishukuru Serikali kwa kazi hiyo. Tulikubaliana kwa sasa wakati tukisubiri mradi huo ukiendelea, tutagawa mita kwa Wananchi wote ili wasitozwe fedha kama *flat rate.* Naomba kujua suala la kuweka mita ya maji limefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Serukamba, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza kwa sababu amekuwa akifuatilia sana Miradi ya Maji Kigoma na hasa huu Mradi mkubwa ambao sasa hivi tayari umeanza na Mkandarasi yuko *site.* Azma ya Serikali ni kwamba, watumiaji wote wa maji walipe *bill* za maji kulingana na wanavyotumia na ili waweze kulipa wanavyotumia ni lazima wafungiwe mita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha bajeti cha mwaka 2012/2013, Mheshimiwa Waziri aliagiza tufunge mita katika Mji wa Kigoma, mpaka sasa tumefunga mita 1,400 ambazo zinafanya kufikia asilimia 64 ya watumiaji wa maji kuwa na mita. Hivi ninavyoongea, tuna mita zingine 700, ambazo zikifungwa tutafikia asilimia 75 ya watumiaji na tutafanya hivyo katika Miji mingine yote ili watu walipe *bill* za maji kulingana na wanavyotumia.

Na. 385

**Matatizo Katika Ofisi ya Uhamiaji Ileje**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. ALIKO N. KIBONA)** aliuliza:-

Ofisi ya Uhamiaji Wilayani Ileje katika Mji wa Isongole inakabiliwa na matatizo mbalimbali kama vile; ofisi kuwa nyumbani kwa mtu na wafanyakazi wake wanashirikiana na mwenye nyumba kupata huduma mbalimbali muhimu; ofisi kuwa ndogo sana watumishi wanabanana wakati wakifanya

kazi zao; wasafiri kulazimika kusimama wakati wakienda kupata huduma ofisini hapo; nyumba hiyo ni mbovu kiasi kwamba mvua ikinyesha hawana pa kujisitiri kwa sababu dari lote la nyumba limeliwa na mchwa na linaweza kuanguka wakati wowote na kusababisha madhara kwa watumiaji wa nyumba hiyo; licha ya hivyo hali ni mbaya kwa afya za Watumishi wa Umma:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa ujenzi unafanyika haraka katika kituo hicho?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kuhusiana na hali ya Ofisi ya Uhamiaji Ileje katika Mji wa Isongole kuwa ni mbaya kutokana na ukweli kwamba, ilikuwa ni vigumu kupata Ofisi zenye hadhi na ubora katika Wilaya ya Ileje wakati tunaanzisha Kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hali hiyo, Idara ya Uhamiaji imefanya juhudi za kutafuta kiwanja katika Wilaya hiyo na kukilipia. Suala la ujenzi wa ofisi hiyo lipo katika mpango wa ujenzi wa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 kwa kutumia Mfuko wa Nyumba wa Idara ya Uhamiaji.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake.

(i) Kwa kuwa na yeye pia anakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, jengo hilo liko kwenye hali mbaya, ofisi ndogo, paa linavuja, watumiaji wanabanana na wamepanga nyumbani kwa mtu na wanashirikiana na huyo mtu; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema wakati huo pale Isongole hapakuwa na nyumba zenye hadhi ya kupanga: Je, sasa atakuwa tayari kwa sababu ya hali mbaya

ya jengo hilo wakati wakisubiri kujenga jengo la kudumu, watafute nyumba nzuri ambapo watumishi watakaa kwenye hali nzuri zaidi?

(ii) Wilaya ya Ileje imeanzishwa mwaka 1975 mpaka leo hawana jengo na Waziri anasema wamepata kiwanja hivi karibuni na kwamba wapo kwenye mpango wa kujenga kwa mwaka 2013/2014. Anatuhakikishia sasa au anawahakikishia Wanaileje na Wanaisongole ni lini jengo hilo litakamilika ili waanze kulitumia jengo ambalo linastahili kwa Watumishi wa Serikali kulitumia?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tutaliangalia jengo na kuangalia muda ambao tutatumia kumaliza hilo jengo jipya kuona kama uwiano wake una masilahi ya kiuchumi kwetu na tutatekeleza kuona kwamba watu wetu pale wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la muda wa kukamilika. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Zambi na Wakazi wa Ileje kwamba, tutafanya kila jitihada kuhakikisha jengo hili linakamilika mapema ili kazi zetu ziweze kufanyika kwa ufanisi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mafupi kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, niliyemwona akisimama wakati wa swali la msingi alikuwa Mheshimiwa Mhonga.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la kutokuwa na Vituo au Ofisi za Polisi zenye hadhi lipo nchi nzima na vilevile tatizo la ukosefu wa nyumba za askari pia ni tatizo ambalo ni sugu sana nchi nzima. Nataka tu kufahamu Serikali imejipangaje ili kuondoa matatizo haya

sugu ambayo miaka yote tunaongea lakini utekelezaji haufanyiki?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nyumba za askari kwa ujumla wake tunalitambua na hivi sasa tumeanza kuchukua hatua, ikiwemo kushirikiana na nchi rafiki, kuona tunavyoweza kulipunguza au kulimaliza kabisa. Kwa hiyo, tunaomba mtupe muda, tutafanya kazi yetu inavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mafupi, lakini yanayotoa maelezo sahihi ya maswali.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Naomba nitoe matangazo niliyonayo; kwanza, tunao wageni waliokuja kututembelea Bungeni asubuhi hii. Pale kwenye Jukwaa la Spika yuko Bibi Sheila Hatimu, yeye ni Msaidizi wa *Serjeant-At-Arms* kutoka Bunge la Uganda. Bibi Sheila Hatimu tafadhali; nafikiri ameshatoka lakini alikuwa ameingia hapa ndani asubuhi.

Yupo pia Mchungaji Upendo Ngao na mkewe kutoka Usharika wa Makabe KKT Mbezi Jijini Dar es Salaam, wameongozana na Mwinjilisti wa Usharika huo, Bi. Rehema Mwambola; ningeomba na wao wasimame. Tunawashukuru sana Mchungaji, mwendelee kutuombea, liombeeni Taifa, liombeeni Bunge letu na tuombeeni Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuwa na afya nzuri za kuwawakilisha Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 50 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Anna Mkapa Dar es Salaam; naomba wasimame kama wapo.

Tunao wanafunzi 17 na walimu wanne kutoka *Iringa International School* ya Mjini Iringa; naomba wasimame kama wapo hapa ndani.

Tunao wanafunzi 30 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa ya Dar es Salaam; karibuni sana

wanafunzi na walimu, tunashukuru kwa kuja kututembelea na kuona shughuli zetu hapa Bungeni.

Tunao wanafunzi 60 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya *Young Jay* ya hapa Dodoma. Wanafunzi wa *Young Jay* Dodoma karibuni sana, tumefurahi kuwaona ninyi pamoja na walimu wetu.

Tunao wanafunzi 37 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Magereza Moshi; wanafunzi kutoka Moshi tunashukuru sana karibuni.

Tunao wanafunzi 90 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Chamwino Dodoma; tunafurahi sana kuwaona na kwa kweli tunafarijika kwa kuja kututembelea.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi wengine kutoka Zanzibar na wamekuja kama Wageni Maalum wa Wabunge wa Zanzibar, kwa niaba yao Mheshimiwa Samia Suluhu na Mheshimiwa Masoud wanawakilisha na watakuwa na kikao na Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wote, lakini nimeambiwa hawajaingia hapa ndani nadhani watakuwa huko *basement* kwenye ukumbi. Karibuni sana, naomba msimame. Tunafurahi kuwaona, poleni kwa kuvuka bahari lakini hapa Dodoma tuko shuwari.

**WABUNGE FULANI:** Wanatoka *UDOM.*

**MWENYEKITI:** Wanatoka *UDOM!* Tangazo nililotewa nimeambiwa wanatoka Zanzibar; ni wanafunzi wa Zanzibar wanaosoma *UDOM,* lakini wanavuka bahari bado. Kwa hiyo, tumefurahi kuwaona mmevuka bahari mnasoma *UDOM* na tunawatakia mkutano mwema na Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Zanzibar; karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni ambao nimepokea matangazo kwamba wako pamoja nasi leo.

Nina matangazo ya vikao. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter

Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ya kwamba, leo tarehe 11 Juni, 2013 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Namba 227, Jengo la Utawala, saa 7.15 mchana. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Katibu wa Bunge ameniomba niwatangazie kwamba, Wabunge wote wanaarifiwa kuwa, *Toyota Tanzania Limited,* watafanya ukaguzi maalum wa magari aina ya *Toyota* bure. Wawakilishi wao wapo kwenye Viwanja vya Bunge kutoa maelezo juu ya ukaguzi huo, kwa magari yatakayopatikana na matatizo yatatengenezwa na *Toyota* kwa gharama yenye punguzo la asilimia 20. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenye magari yanayotokana na Kampuni ya *Toyota,* mnakaribishwa mwonane na hao wageni wetu ili muweze kupata maelezo na magari yenu yaweze kukarabatiwa tayari kwa kwenda kuwahudumia Wananchi baada ya Bunge hili kukamilika.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho nililonalo hapa linahusu semina. Katibu wa Bunge, ananiomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, shughuli za leo kwa mujibu wa Ratiba ya Bunge, zitakamilika baada ya shughuli ya maswali na baada ya hapo kutakuwa semina itakayohusu Awamu ya Tatu ya Mpango wa *TASAF,* itakayoanza mara tu baada ya kuahirishwa shughuli hizi za Bunge na itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa. Tumesisitizwa Wabunge wote tuhudhurie, kwa sababu semina hiyo ni muhimu sana ili kuweza kubadilishana uzoefu na kupata taarifa za shughuli za *TASAF* katika Majimbo yetu.

Baada ya kusema hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi huu. *(Makofi)*

*(Saa 4. 24 asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 12 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*